

# Kelele Ya Usiku wa Manane wa Kweli

Samuel Snow
Adrian Ebens

# Kelele Ya Usiku wa Manane wa Kweli

Tazama Bwana Arusi yuaja, nendeni mkamlaki

Samuel Sheffield Snow

Augosti 22, 1844

Kimechapishwa na

maranathamedia.com

Augosti 12, 2018

## Njia iliyoangazwa

Ellen White anaelezea kusonga kwa roho kuwa kama wimbi la bahari katika mwitikio wa Kelele ya usiku wa Manane wa harakati ya mwezi wa saba. Watu wachache hutambua jinsi harakati hiyo ilikuwa yenye nguvu. Zingatia kwa makini maneno:

> Tumaini letu sasa likizingatiwa kwa kuja kwa Bwana katika mwaka wa 1844. Huu pia ulikuwa wakati wa ujumbe wa malaika wa pili, ambaye, aliruka katikati ya mbingu, akisema, "Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa." Ufunuo 14:8. Ujumbe huo ulihubiriwa mwanzo na watumishi wa Mungu katika majira ya kiangazi ya 1844. **Kwa sababu hiyo, wengi walitoka katika kanisa lililoanguka. Kwa kuunganisha pamoja na ujumbe huu "kelele ya usiku wa manane" [Tazma Mathayo 25:1-13.] ilitolewa:** "Tazameni, huyu hapa Bwana arusi! Tokeni nje mkamlaki." **Katika kila sehemu ya inchi nuru ilitolewa kuhusiana na ujumbe huu, na kelele iliwaamsha maelfu. Ilienda kutoka mji hadi mji, kutoka vijiji hadi vijiji, na hata katika sehemu za mashambani**. Iliwafikia wenye elimu na wenye talanta, na vile vile walio gizani na wanyenyekevu. **Huu ulikuwa mwaka wa furaha zaidi katika maisha yangu**. Moyo wangu ulijawa matarajio makuu; {CET 50, 51}
>
> **Siku ya kumi ya mwezi wa saba, Siku kuu ya Upatanisho, wakati wa patakatifu kutakaswa, ambayo katika mwaka wa 1844 ilianguka katika tarehe**. Hili lilikuwa kwa uiano na ithibati ambayo tayari ilikuwa imewasilishwa kwamba siku 2300 zitaishia katika majira ya vuli, na hitimisho ilionekana isiyo na pingamizi.
>
> Katika mfano wa Mathayo 25 wakati wa kusubiri na kusinzia unafuatwa na kuja kwa Bwana arusi. **Hili lilikuwa kulingana na hoja zilizowasilishwa, kutoka kwa unabii na mifano. Walibeba imani thabiti ya ukweli wao; na "kelele ya usiku wa manane" ilihubiriwa na maelfu ya waumini**.
>
> Kama mawimbi ya bahari harakati iliifagia nchi. Kutoka mji hadi mji, kutoka kijiji hadi kijiji, na katika sehemu za mashambani ilifika, hadi watu wa kusubiri wa Mungu wakaamshwa. Ushabiki ulipotea kabla ya tangazo hili kama baridi ya awali kabla ya jua kuchomoza. Waumini waliona shaka yao na mshangao ukiondolewa, na tumaini na ujasiri zilihuisha mioyo yao. GC 399,400

**Katika harakati zote kuu za kidini tangu siku za mitume, hakuna ambayo imekuwa huru kutoka kwa kasoro za wanadamu na hila za Shetani kuliko ilivyokuwa ile ya vuli ya 1844.** Hata sasa, baada ya miaka mingi kupita, wote ambao walishiriki katika harakati hiyo na ambao wamesimama dhabiti juu ya jukwaa la kweli bado wanahisi athari takatifu ya kazi hiyo ambayo imebarikiwa na kushuhudia kwamba ilikuwa ya Mungu. GC 402

Harakati hii ilisababishwa na hati ifuatayo ilioandikwa na Samuel Snow ambayo ilichapishwa kwa mara ya kwanza Julai 21, 1844. Iliweka wazi mbele ya watu wa Mungu wakati wa siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Bibilia, ambao ulikuwa Oct 22, 1844. J.N. Loughborough anarekodi tukio ambalo lilisababisha kelele ya usiku wa manane:

Kwa hivyo mgogoro uliendelea hadi Julai 1844, wakati ambao mkutano mkuu wa makambi ambao ulufanywa na Waadventista, walikusanyika katika Exeter, N.H sawa. Ilirepotiwa kwamba kulikuwa na watu elfu tatu katika kambi hiyo. Ilifanyika kwenye miti, mahali wazi, hakukuwa na banda la kuvalia kwa huduma ya makambi, lakini viti vingi. Jumapili jioni Mzee wa kanisa Joseph Bates alikuwa akihubiri, mtu mmoja alipoingia kwenye kambi akiendesha farasi kwa kasi, akaweka farasi wake walipokuwa wakiweka mifugo yao, kisha akaja kwenye hadhira, na akaketi karibu na familia ya mzee John Couch, na kwa Bibilia wazi, kwa mnong'ono, aliwaelezea kisababishi cha kukatishwa tamaa, na kelele ya usiku wa manane ambayo sasa ilikuwa imeisha..

Ndugu Bates alikuwa akitumia kama mfano wa mwendo wao katika kungoja kwa subira, uzoefu wake wa kukaribia nyumbani katika safari ya bahari, baada ya kukosekana kwa muda mrefu. Nguvu za Mungu zilimjia Dada Couch, aliposimama, na kumpa ishara Ndugu Bates. Alisema, Dada, kuna nini?" Alijibu, kile ambacho unasema ni kizuri, lakini kuna mtu aliye na nuru juu ya kelele ya usiku wa manane." "Vyema," akasema ndugu Bates, "basi wacha aje kwenye jukwaa, na aipeane kwa watu," na akaketi.

Muhudumu ambaye alitembea kwelekea kwenye jukwaa alikuwa S. S. Snow, ambaye katika sentensi chache aliwapa njia ya ujumbe wake wa kelele ya usiku wa manane. Mzee James White alikuwa katika hadhira hiyo; sikuwa pale, lakini nilipata nuru kuhusiano na suala hilo kutoka kwa wale waliokuwepo.

Kelele ya Usiku wa Manane

Ndugu Snow kwa hivyo aliwauliza maswali; "Tumefikia wapi katika uzoefu wetu wa Ujio?"

Jibu kutoka kwa hadhira: "katika wakati wa kukawia."
Swali: "maono hayo yalikuwa yakawie kwa kipindi kipi?"
Jibu: "Hadi kelele ya usiku wa manane"
Swali: "Siku ni nini katika unabii?"
Jibu: "Mwaka."
Swali: "Basi usiku utakuwa nini?"
Jibu: "Miezi sita."
Swali: "Basi usiku wa manane utakuwa nini?"
Jibu: "Miezi tatu."
Swali: "Tumekuwa katika kukawia kwa kipindi kipi?"
Jibu: "Miezi mitatu tu."

Alisema, "basi sasa ni usiku wa manane, na niko hapa na kelele ya usiku wa manane." katika sentensi chache alielezea kwamba ilikuwa katika anguko la 457 ambapo amri ilitolewa, na kwa hivyo walipungukiwa miezi sita katika kuhesabu kwao, akiwaonyesha kwamba siku 2300 zitaisha Oct. 22, 1844, badala ya wakati wa machipuko kama walivyokuwa wamefikiria hapo awali. Na kisha kwa sauti yenye nguvu alisema, "Tazama Bwana harusi anakuja katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, Oct. 22, 1844. Tokeni mkamlaki."

Alipotamka maneno hayo nguvu za Mungu ziliijaza kambi hiyo, ikiwaangusha wengi chini, ghafla ikigeuza kambi hiyo kuwa mkutano wa muungamo wenye msukumo na ushuhuda. Huo ulikuwa mwanzo tu wa ujumbe wa kelele ya usiku wa manane, karatasi ambayo alikuwa mhariri, "Ilifagia nchi kwa kasi ya tornado, na ilifikia mioyo katika semu tofauti na mbali, karibu kwa wakati huo huo, na kwa namna ambayo inaweza semwa tu kwa dhana kwamba Mungu alikuwa ndani yake." J.N. Loughborough, *The Great Second Advent Movement*, p 523

## Malaika aliponena kwa Ellen White akielezea tukio lililopelekea kwa kukatishwa tamaa kwa Oct 22, 1844, aligundua:

Nilipokuwa nikiomba katika madhabahu ya familia, Roho Mtakatifu alikuja juu yangu, na nilionekana kuinuka juu zaidi, juu kuliko ulimwengu wa giza. Niligeuka kutafuta Waadventista ulimwenguni, lakini sikuwaona, ndipo sauti ikasema kwangu, "Angalia tena, na angalia juu kidogo." Katika hili niliyainua macho yangu, na nikaona njia iliyonyooka na nyembamba, ikiwekwa juu ya ulimwengu. Juu ya njia hii Waadventista walikuwa

> wakisafiri kwelekea kwenye mji, ambao ulikuwa mbali kwenye mwisho wa njia. **Walikuwa na mwanga uliong'aa uliowekwa nyuma yao kwenye mwanzo wa njia, ambao malaika aliniambia ulikuwa kelele ya usiku wa manane**. Nuru hii iliangaza njia yote na kutoa nuru kwa miguu yao ili kwamba wasijikwae. EW 14

Ujumbe wa kelele ya usiku wa manane uliotolewa na Samuel Snow Julai ya mwaka wa 1844 ulikuwa na habari ambayo ingeangaza njia ya watakatifu katika safari yote ya kuelekea mji wa Mungu. Kadri walivyodumisha macho yao kwa Yesu wakijihami na habari hii hawangejikwaa. Ujumbe wa kelele za usiku wa manane ulikuwa na habari kuhusu yafuatayo

1. Miaka 6000
2. Miaka 2520 ya unabii
3. Miaka 2300 ya unabii
4. Majuma sabini ya Danieli Tisa
5. Mwaka wa Kusulibiwa ukiwa AD 31
6. Ijumaa ndio siku ambayo Kristo alikufa mwaka huo.
7. Kalenda ya Wayahundi wa Karaite (Karaite Jewish) ikiwa kalenda sahihi ya kutambua sherehe za kibibilia na kwa hivyo kuamua tarehe Oct 22, 1844 kama tarehe ya siku ya upatanisho mwaka huo.
8. Kutolewa kwa sheria Mlima Sinai kulikuwa mfano wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika siku ya Pentekosti.
9. Kuja kwa Kristo kumeshikamanishwa na Jubilee na kisha mfano wa sikukuu ya vibanda itatendeka pamoja na karama ya harusi ya Mwana-kondoo.
10. Kipindi cha miaka 1000 baada ya kuja kwa Kristo ni Sabbato ya Milenia ya Pumziko.

Nguvu hii ya roho ambayo ilihudhuria kelele ya usiku wa manane kwa ushirikiano na ujumbe wa malaika wa pili inatukaribisha kuangazia kwa makini jinsi hoja za ujumbe huu zimewekwa dhabati. Kuzipuuza ni kuchujuka nuru ambayo huangaza "njia yote", jambo ambalo linaweza tufanya tuanguke kutoka kwa njia iliyonyooka na nyembamba ya kuelekea kwa uzima wa milele.

Maana ya Kalenda ya Karaite haikomei tu katika jinsi ya kuanza mwaka wa kibibilia, inatwambia pia kwamba siku ya saba ya juma ni Sabbato – akwa hivyo kuondoa dhana kwamba Sabbato inahesabiwa kulingana na Mwezi Mpya au Sabbato ya Mzunguko wa jua. Pia inaondoa dhana kwamba Sabbato huanza alfajiri, kwa vile sio sehemu ya mfumo wa kalenda ya Karaite.

Wito wangu wa bidii kwa wale wenye mvuto kwa ujumbe wa malaika wa tatu ni kusikiliza kelele ya usiku wa Manane na kudumu kwenye njia ambayo imeangazwa kwa ajili yetu kwelekea kwenye mji. Kuna sauti nyingi ambazo zinawaita watu wa Mungu kuacha kelele ya usiku wa manane, lakini wito wote kama huo utaishia kwenye uharibifu. Wenye masikio ya kusikia, na asikie.

## Kelele za usiku wa Manane za Kweli na Samuel Snow

Mfalme wetu na Bwana ameahidi kwamba atarudi tena na kupokea watu wake kwake; ili alipo, wawe pia. Mahali ambapo yeye na wao wataishi milele, ni Yerusalemu Mpya, mji huo mtakatifu, ambao Mungu ameandaa kwa ajili yao, na ambao utashuka kutoka kwa Mungu mbinguni, na Nchi hiyo Mpya, ambapo watakatifu wanakaa ndani yake.

Kuhusiana na wakati wa kuja hukwo, anasema, katika Marko 13:32, "Lakini kwa habari ya siku ile na saa hakuna ye yote ajuaye, hata malaika walioko mbinguni wala hata Mwana hajui, ila Baba peke Yake." Inadhahaniwa na wengi, kwamba fungu hili linadhibitisha kwamba kamwe watu hawatajua wakati. Lakini kama linadhibitisha hili, vile vile linadhibitisha kwamba Mwana wa Mungu mwenyewe kamwe hatajua wakati: kwa kuwa fungu linatangaza wazi sawa kuhusiana naye jinsi linavyo kuhusiana na malaika na wanadamu. Lakini mtu yeyote anaweza amini kwamba Bwana wetu mtakatifu, ambaye amepewa uwezo wote mbinguni na duniani, hajui, na atasalia kutojua wakati hadi saa ile ambayo atakuja kuhukumu ulimwengu? Kama sivyo, basi bila shaka jaribio hili kamwe haliwezi dhibitisha kwamba wanadamu hawawezi fanywa kufahamu wakati. Tafsiri ya kale ya kifungu hiki inasema, "Lakini habari za siku ile na saa hakuna yeyote afanywaye kujua, wala malaika walioko mbinguni, wala Mwana, ila Baba." Huu ndio usomi sahihi kulingana na wakosoaji wenye uwezo wa kale. Neno kujua limetumika hapa na maana sawa kama ilivyo na Paulo katika 1 Kor. 2:2. Paulo alifahamu vyema vitu vingine vingi kando na Kristo na yeye aliyesulubiwa, lakini aliamua kufanya chochote kutojulikana miongoni mwao. Kwa hivyo katika kifungu kilichonukuliwa mwanzo, imetangazwa kwamba hakuna yeyote ila Mungu Baba hufanya ijulikane siku ile na saa, huo ni, wakati halisi wa kuja mara ya pili kwa Mwanawe. Na hili lazima linapendekeza kwamba Mungu hufanya wakati ujulikane.

Agano la Kale lina ushuhuda wa Baba kuhusiana na Mwanawe, na kuhusiana na wakati wote wa kuja kwake mara ya kwanza na mara ya pili. Kwa hivyo wakati utafahamika. Tazama Dan. 12:10, "Wengi watajitakasa, na kujifanya weupe, na kusafika; bali wabaya watatenda mabaya; wala hataelewa mtu

mbaya awaye yote; bali wao walio na hekima ndio watakaoelewa." Rum. 15:4, "Kwa maana kila kitu kilichoandikwa zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili kwamba kwa saburi na faraja tunayopata katika Maandiko tuwe na tumaini." Ni kwa mafundisho ya neno lake, kama tunavyoongozwa na Roho Mtakatifu, tunaweza kufahamu wakati wa kuja kwa Mfalme wetu Mtukufu.

Kama dhibitisho zaidi kwa hili, tazama Dan. 9:25, "Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu." Marko 1: 14-15, "Baada ya Yohana kukamatwa na kutiwa gerezani, Yesu aliingia Galilaya akaanza kuhubiri Habari Njema za Mungu, akisema, “Wakati umewadia." Luka 19:43-44, "Hakika siku zinakujia, ambazo adui zako watakuzingira, watakuzunguka pande zote na kukuzuilia ndani. Watakuponda chini, wewe na watoto walioko ndani ya kuta zako. Nao hawataacha hata jiwe moja juu ya jingine, kwa sababu hukutambua wakati wa kujiliwa kwako." 1 Pet. 1:9-11, "Maana mnaupokea wokovu wa roho zenu, ambao ndio lengo la imani yenu. Kwa habari ya wokovu huu, wale manabii walosema kuhusu neema ambayo ingewajia ninyi, walitafuta kwa bidii na kwa uangalifu mkubwa, wakijaribu kujua ni wakati upi na katika mazingira gani ambayo ndani yao Roho wa Kristo aliyokuwa akionyesha alipotabiri kuhusu mateso ya Kristo na utukufu ule ambao ungefuata." Isa. 40:1-5; Matendo 17:30, 31, "Kwa kuwa ameweka siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki." Muhubiri. 3:17, "Mungu atawahukumu wenye haki na wasio haki; kwa kuwa kuna wakati huko kwa kila kusudi na kwa kila kazi." Muhubiri. 8:5-7, "Aishikaye amri hatajua neno baya; Na moyo wa mwenye hekima hujua wakati na hukumu." Yer. 8:6-9, "Nalisikiliza nikasikia, lakini walisema yasiyo sawa; hapana mtu aliyetubia maovu yake, akisema, Nimefanya nini? Kila mtu hurudia mwendo wake mwenyewe, kama farasi aendavyo kasi vitani. Naam, koikoi angani ajua nyakati zake zilizoamriwa; na hua na mbayuwayu na korongo huangalia wakati wa kuja kwao; bali watu wangu hawazijui amri za Bwana. Mwasemaje, Sisi tuna akili, na torati ya Bwana tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo. Wenye hekima

wametahayari, wamefadhaika na kushikwa; tazama, wamelikataa neno la Bwana, wana akili gani ndani yao? Hosea 9: 7-9, "Siku za kupatilizwa zimekuja, siku za kulipa zimefika; Israeli atayajua hayo; huyo nabii ni mpumbavu, huyo mtu mwenye roho ana wazimu; kwa sababu ya wingi wa uovu wako." Rom, 13:11-14, "Nanyi fanyeni hivi, mkiuutambua wakati tulio nao. Saa ya kuamka kutoka usingizini imewadia.

## Miaka Elfu Sita

Kipindi cha wakati ambacho ulimwengu huu umepewa, katika hali yake ya sasa, ni miaka 6000, na katika kuisha kwake inaanza Sabbato kuu ya milinia inayozungumziwa katika Ufu. 20, na ambayo itakaribishwa na kuonekana kwa Kristo binafsi na ufufuo wa kwanza; tazama Isa. 46:9,10; Mwan. 2:1-3; Ebr. 4:4-9; Isa. 11:10; 2 Pet. 3:8. Kulingana na kronology ya Usher, ambayo kwa kawaida inapokelewa sana, zama za Ukristo zilianza katika mwaka wa ulimwengu 4004; lakini Usher amepoteza katika wakati wa waamuzi miaka 153. Tangia kugawanywa kwa nchi ya Kanani hadi mwanzo wa utawala wa Samweli, anapeana tu miaka 295: ilhali Paulo, katika Matendo 13:20, anatupa “nafasi kama ya 450.” Kutoka kwa kitabu cha Waamuzi tunapata miaka 430, na Yoshephati anatupa 18 zaidi ya wazee na machafuko, kabla mwamuzi yeyote kutawala; hii ikiongezwa kwa 430 inakuwa 448 ambayo inakubaliana na Paulo, ikipendekeza kwamba alikuwa amezungumza kwa nambari kamili. Tofauti kati ya wakati huu na ule ambao ulipeanwa na Usher ni miaka 153, na lazima iongezwe kwa miaka ya ulimwengu, ikifanya mwanzo wa zama za Ukristo 4157, au, kwa njia nyingine, au 4156 na sehemu ilikuwa imepita katika wakati uliopendekezwa wa kuzaliwa kwa Kristo. Ukiondoa hii kutoka kwa miaka 6000, inabaki 1843 na sehemu. Kwa hivyo kipindi kitaishia katika A. D. 1844.[1]

[1] Samuel Snow alikosea katika hesabu yake ya kukamilika kwa miaka 6000 ingawa kutumia kakamilika kwa miaka 6000 kama sehemu ya ushahidi wa kujiandaa kwa kuja kwa Bwana wetu kunasalia. Miaka 6000, kuja kwa Yesu na ufufuo wa kwanza, na kisha Sabbato ya miaka 1000 kabla ya ufufuo wa pili.

## Nyakati Saba za watu wa Mataifa (2520)

Nyakati saba za utawala wa watu wa Mataifa juu ya kanisa la Mungu, zinazozungumziwa katika Law. x xvi., zilianza kwa kuvunjwa kwa kiburi cha uwezo wao. Katika kushikwa mateka kwa Manasseh, mfalme wa Yuda, B. C. 677. Tazama Isa. 10:5-12. Yer. 15:3-9; Yer. 1:17; 2 Nyak. 32:9-11. Hii ndio tarehe iliyowekwa na wapangiliaji kwa tukio hilo. Nyakati saba za unabii ni miaka 2520. Kama dhibitisho ya hili, tazama Ufunuo, 12:6,14, ambapo nyakati 3½ ni sawa na miaka 1260. Hivyo wakati una miaka 360 ya mzunguko wa jua, ambazo zikizidishwa na 7, zinatupa 2520. Kama kipindi hiki kilianza na siku ya kwanza ya B.C. 677, kingekamilika na siku ya kwanza ya A. D. 1844, kwa vile miaka 677 kamili kwa upande mmoja, na 1843 kwa upande mwingine, inakuwa miaka 2520 kamili. Inadhaniwa kwamba kipindi kitaishia katika A. D. 1843. Lakini sehemu ya B.C. 677 inapowachwa nje, sehemu sambamba ya A. D. 1844 lazima iongezwe ili kukamilisha kipindi hicho. Lazima Mannaseh alipelekwa mateka katika wakati wa vuli. Kama dhibitisho ya hili, Tazama Hosea 5:5; Isa 8:8; Isa 10:11. Hosea anatangaza kwamba Ephraim na Israeli zitaanguka, na kwamba Yuda pia itaanguka pamoja nazo; Isaya anamwasilisha mfale wa Ashuri akitishia kuifanyia Yerusalemu alivyo ifanyia Samaria; kwa hivyo kutawanywa kwa mwisho kwa kabila kumi kulikuwa kabla ya kuvamiwa kwa Yuda, na katika mwaka huo huo. Unabii wa Isa. 7:8, umewekwa kwa usahihi B.C. 742; miaka 65 tangia sehemu hiyo inatufikisha B.C. 677. Katika mwaka huo kulikuwa na kuvunjwa kwa mwisho kwa Ephraim, kwamba kusiwe na watu. Historia ya hili tunaipata katika 2 Wafalme, sura ya 17. Wafalme hawakuenda mbele katika misafara yao ya kivita majira ya vuli au baridi, bali majira ya machipuko au kiangazi. Kwa hivyo majira ya machipuko au kiangazi ya B.C. 677, Esarhaddon, na Ashuri walianza kuondoa masalio ya kabila kumi kwenye mji wa Samaria; na walipokuwa wamekamilisha hili, waliwaleta wageni na wakawaweka pahali pao, kunyakua miji hiyo. Baada ya kutekeleza kazi hii, ambayo ilichukua miezi kadhaa, wlikuwa tayari kuvamia Yuda. Hivyo katika majira ya vuli ya B.C. 677 walichukua mji wa Yerusalemu, na wakamfunga mfalme wake kwa pingu na wakambeba hadi Babeli. Tangu wakati huo miaka 2520 ilifika kwa majira ya vuli ya A.D. 1844. Kisha nyakati za Mataifa zingekamilishwa, mpangilio wa utimilifu wa nyakati utakuja, Mkombozi atakuja Zayuni, na Israeli yote itaokoka.

## Siku 2300

Siku 2300 za Dan. 8:14 zimetolewa kama urefu uliopo katika sura hiyo. Beberu ni waamedi na wajemi, mbuzi ni Uyunani, na pembe mdogo aliyenena makuu ni Roma. Kuanzia sura ya pili na saba ya Danieli tunajifunza kwamba Roma itafikia mwisho wake wakati Mzee wa siku atakapokuja, hukumu inawekwa, Mwana wa Adamu anakuja katika mawingu ya mbinguni, na Mungu wa mbinguni anaweka ufalme wa milele. Kwa hivyo siku 2300, ambazo zinaendelea hadi wakati ambao pembe mdogo aliyenena makuu "atavunjwa bila kazi ya mikono," hadi "mwisho wa ghadhabu" ni miaka mingi sana, na inamalizika wakati wa kuja kwa Yesu katika Mawingu ya Utukufu. Kipindi kilianza kwa majuma 70 ya Dan. 9:24, ambayo yameamriwa, au kutengwa, na yanajumuisha sehemu ya siku 2300. Kwa hivyo lazima yaanze pamoja. Kwanzia fungu la 25, tunagundua kwamba zinaanza katika amri ya kurejesha na kujenga Yerusalemi. Pahali pa kuanza kuhesabu wakati, lazima pawe wakati ambao amri ilitolewa mwanzo au wakati ambao ilianza kutekelezwa; haiwezi kuwa ya awali, kwa sababu amri inakumbatia yote ambayo yaliamriwa na Cyrus, Darius, na Artashasta, wafalme wa Uajemi. Tazama Isa. 44:23; Isa. 45:13; 2 Nyak. 36:22, 23; Ezra 1:14; Ezra 6:1-15; Ezra 7. Amri inakumbatia mambo matatu makuu: kujengwa kwa Hekalu, kurejesha umoja wa Wayahudi, na kujengwa kwa mitaa na ukuta. Sasa kama majuma 70, ambayo yanajumuisha miaka 490, kama ilianza na kutolewa mara ya kwanza kwa amri, B.C. 536, yangeisha B.C. 46; lakini majuma 69 yangeendelezwa kudhihirisha kwa masihi, na la 70, au la mwisho, linajumuisha wakati wa kusulubiwa; kwa hivyo lazima tuhesabu kutoka hatua hiyo nyingine, ambayo ni, kupitishwa na kutekelezwa kwa amri Judea..

Kutoka kwa Ezra 7:8, 9, tunagundua kwamba Ezra alianza kukwea siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza, na akafika Yerusalemu siku ya kwanza ya mwezi wa tano, katika mwaka wa 7 wa Artashasta, B.C. 457. Baada ya kufika Yerusalemu, aliteua mahakimu na waamuzi, na akarejesha umoja wa Wayahudi, chini ya ulinzi wa Mfalme wa Uajemi, kama alivyokuwa ameagizwa kufanya kikamilifu na amri ya Artashasta. Hili bila shaka lilihitaji muda mchache, na linatuleta pahali ambapo, baada ya marejesho kutekelezwa, kujengwa kwa miji na ukuta kulianza. Majuma 70 yamegawanywa katika

sehemu tatu: majuma 7, majuma 62, na juma 1- tazama Dan. 9: 25. Mshikamano unaonyesha kwamba majuma 7 yalipeanwa kwa ujenzi wa miji na ukuta. Kwa hivyo yalianza walipoanza kujenga, majira ya vuli ya B.C. 457; tangu hapo miaka 2300 inafika hadi majira ya vuli ya A.D. 1844.

## Majuma Sabini

Majuma 69 yanaendelea hadi kudhihirishwa kwa Masihi. Imedhaniwa na wengi kwamba hili lilikuwa wakati wa ubatizo wake, lakini hili ni kosa, kama inavyoonekena kikamilifu kutoka kwa Yohana 1: 19-34. Hapo tunagundua, kwamba baada ya kubatizwa kwa Kristo hakuwa anajulikana na wayahudi kama Masihi; Yohana anasema, fungu 26, "Lakini katikati yenu yupo mtu msiyemjua;" na katika fungu la 33, 34, anatangaza kwamba hakumjua, hadi alipoona Roho akishuka na kusalia juu yake katika ubatizo wake, ambaye alikuwa kabla yake kutoa ushahidi huu. Hakuna dhibitisho kwamba yeyote aliona roho akishuka isipokuwa Yohana. Kwa hivyo dhibitisho hili kwamba Yesu alikuwa Masihi, halikupeanwa kwa yeyote ila Yohana, isipokuwa ulipeanwa kwa wengine katika ushuhuda wa Yohana. Lakini ushuhuda wa Yohana haukutosha kikamilifu kuanzisha pahali; kwa sababu anatangaza, Yohana 5:33,34 "Mlituma wajumbe kwa Yohana, naye akashuhudia juu ya kweli. Si kwamba naukubali ushuhuda wa mwanadamu, la, bali ninalitaja hili kusudi ninyi mpate kuokolewa."

Katika fungu la 36 Kristo anasema, "Lakini ninao ushuhuda mkuu zaidi kuliko wa Yohana. Kazi zile nizifanyazo, zinashuhudia juu yangu, zile ambazo Baba amenituma nizikamilishe, naam, ishara hizi ninazofanya, zinashuhudia kuwa Baba ndiye aliyenituma." Miujiza ya Kristo inamthibitisha kuwa Masihi; lakini hata ushuhuda wake mwenyewe bila miujiza hiyo haukutosha kuonyesha mahali, kama ilivyodhahiri katika fungu la 31: "Kama ningejishuhudia Mimi mwenyewe, ushuhuda Wangu si kweli." Miujiza ya Kristo aliyoifanya kwa umma haikuanza hadi baada ya Yohana kutiwa gerezani --tazama Mat. 11:2-6; Luka 7:19-23 unabii wa Dan. 9:25 kuhusiana na majuma 69, yalikuwa yamekusudiwa kwa taifa lote la Wayahudi; na walihukumiwa kwa sababu hawakujua. Katika Luka 19:43,44, tunapata Bwana wetu akitangaza juu yao hukumu ya kutisha kwa sababu hawakujua wakati wa ujio wao. Unabii

ulikuwa wazi, na wangeusikia. Mkombozi wetu, pia aliwaambia wazi wakati ambao kipindi kiliisha, akisema, "Wakati umetimia." Tazama Marko 1:14, 15; Matt. 4:12, 17; Matendo 10:37; hivyo tunaona kwamba majuma 69 yalikamilika, na juma la 70 likaanza, muda mfupi baada ya Yohana kutiwa gerezani. Yohana alianza kazi yake katika mwaka wa kumi na tano wa Tiberio Kaisaria –tazama Luka 3:1-3. Utawala wa Tiberio ulianza, kulingana na ushuhuda wa pamoja wa wana-kronology, katika Aug. A.D. 26, mwaka wake wa kumi na tano ulipoanza. Kazi ya Yohana, kwa hivyo, ilianza katika sehemu ya mwisho ya A.D. 26. Kutoka Luka 3:21, tunagundua kwamba baada ya Yohana kuwa akibatiza kwa muda, Yesu alikuja na akabatizwa; na fungu la 23 linatufahamisha kwamba wakati huo hakua mbali na umri wa miaka 30. Imedhibitishwa angani kwamba Mkombozi wetu alizaliwa miaka nne kabla ya kipindi cha Ukristo. Ithibati ni hii. Kama mwaka wa 527, Dionysius Exigus, mtawala wa Rumi aliweka mwanzo wa kipindi cha Ukristo katika mwaka wa kipindi cha Juliani 4713. Kuhesabu huku kumefuata hadi wakati wa sasa. Lakini Yosephus, katika mambo yake ya kale, kitabu cha 17, sura ya 6, anataja hasa kupatwa kwa mwezi, ambako kulitendeka muda mfupi kabla ya kifo cha Herode; na jedwali za kianga zinathibitisha kupatwa huku kulikuwa Marchi, 13, katika mwaka wa kipindi cha Juliani 4710. Bwana wetu miezi kadhaa kabla ya hili; kwa sababu baada ya kuzaliwa kwake Herode alitafuta kuangamiza maisha yake, na Yusufu, kwa kutahadharishwa na malaika wa Bwana katika ndoto, alimchukua mtoto mchanga na mamaye, na akaenda Misri, ambapo alikaa hadi baada ya kifo cha Herode--tazama Matt. 2:13-15. Sehemu ya mwisho, kwa hivyo, ambayo tunaweza weka juu ya kuzaliwa kwa Kristo, ni karibu na mwisho wa mwaka 4709, miaka minne tu mbele ya pahali pa wakati uliotolewa na Dionysius ya kuanza kwa kipindi cha Ukristo. Kwa hivyo, Yesu alikuwa umri wa miaka 30 karibu na mwisho wa A.D. 26, na katika ubatizo wake alikuwa zaidi kidogo ya 30. Muda mfupi baada ya hili, kama ilivyothabiti katika Yohana 2:11-13, kulikuwa na pasaka. Hii, ikiwa pasaka ya kwanza baada ya ubatizo wa Yohana, lazima ilikuwa katika majira ya machipuko ya A.D. 27. Baada ya hili Yesu alikuwa na mahojiano yake na Nikodemu na akamfundisha kuhusiana na kuzaliwa upya--Tazama Yohana 3:1-21. Katika fungu 22 tunafahamishwa kwamba Yesu alirejea, baada ya mambo haya, katika nchi ya Judea, ambapo alikaa na kubatiza. Kama alivyokuwa awali katika Yerusalemu wakati wa pasaka--tazama Yohana

2:23—na sasa alirejea Judea, lazima hakuwepo katika nchi hiyo kati ya wakati huu wote. Hili bila shaka linatuleta katika majira ya joto au vuli ya A.D. 27. Lakini "Yohana hakuwa ametupwa gerezani bado"—tazama Yohana 3:24. Kwa hivyo tunalazimishwa kuweka upeo wa wakati ambao Yesu alianza kutangaza injili Galilaya, katika vuli ya A.D. 27. Hapa majuma 69 yalikamilika, na hapa juma lilianza, ambalo anafanya agano--tazama Dan. 9:27. Katika nusu ya juma Yesu alifanya sadaka na dhabihu kukoma kwa kujitoa kama Mwana-kondoo, asiye kuwa na mawaa, kwa Mungu msalabani. Neno la Kiebrania likitafsiriwa “nusu,” naye Lexicon akielezea, "nusu, sehemu nusu, kati, nusu." Juma liligawanywa katika nusu mbili, na tukio ambalo lilikuwa liligawanya lilikuwa kifo cha Kristo.

## Kalenda Ya Karaite

Tukio hili lilitendeka, kulingana na Dkt. Hales, mmoja wa wana-kronology bora katika majira ya machipuko ya A.D. 31. **Ferguson ameliweka katika A D. 33; lakini ili kuthibitisha hili anachukua mbinu ya Marabii ya kuhesabu mwaka, ambayo sio sahihi. Walianza mwaka kwa upya katika mwezi katika Marchi; lakini Karaiti na mwezi mpya katika Aprili. Neno Karaiti linaashiria “Aliyemkamilifu katika sheria.” Hili linawashtaki Marabii kwa kuondoka kwenye sheria, na kuzichukua mila za mataifa; na madai tu ni wanasimamisha mwaka wao kwa ikimtia, katika kuwaiga Warumi; ila sheria haisemi chochote cha ikimtia;**[2] bali ilihitaji, katika siku ya 16 ya mwezi wa kwanza[3], sadaka ya malimbuko ya mavuno ya shayiri. Lakini kama kwaka ukianza kulingana na Marabii na mwezi mpya katika Marchi, mazoa ya shayiri hayawezekani kuwa yameiva katika siku 16 tangu wakati huo. **Karaite kwa hivyo bila shaka wako sahihi. Sasa Bwana wetu alisulubiwa katika siku ya pasaka, kama ilivydhabiti katika Yohana 18:28. Vile vile ilikuwa siku kabla ya Sabbato, kama inavyodhibitishwa kutoka kwa Yohana19:31. Kulinga na**

---

[2] Kwa taarifa zaidi kuhusiana na hili tazama “*The Seventh Month Movement, the Midnight Cry and the Karaite Calendar*.”

[3] Samuel Snow anatoa wazo kwamba Kalenda ya Karaite inahesabu kupunga kwa malimbuko katika siku ya 16 lakini hili sio sahihi. Snow anatambua kalenda sahihi lakini anaiunganisha na hesabu ya Rabii ya malimbuko ambayo sio sahihi. Tazama https://www.nehemiaswall.com/truth-shavuot kwa maelezo zaidi. Tazama pia mahubiri, Kalenda na Upatanisho.

**kuhesabu kwa Marabi, pasaka ilifanyika siku kabla ya Sabbato katika A.D 33, na sio kwa miaka kadhaa kabla na baada. Lakini kulingana na kuhesabu kwa Karaite, pasaka ilitendeka siku hiyo katika A. D. 31**. Kwa hivyo huo ulikuwa mwaka wa kusulubiwa. Agano lilithibitishwa kwa nusu juma na Kristo, na nusu hiyo nyingine na mitume--tazama Ebr. 2:3,4: "je, sisi tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Wokovu huu, ambao mwanzo ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliomsikia. Pia Mungu aliushuhudia kwa ishara, maajabu na kwa miujiza mbalimbali na karama za Roho Mtakatifu alizozigawa kulingana na mapenzi Yake?" agano ambalo lilithibitishwa ni agano jipya, yaani injili. Kuthibitisha kunasimamia kuianzisha kwa msingi dhabiti. Msingi wa injili, ni Yesu na ufufuo--tazama Matendo 17:18; 1 Kor. 3:9-11; Efe. 2:20. Injili ilijengwa juu ya msingi huu kwa ushuhuda, ukifuatana na miujiza kama ithibati ambazo zilikuwa muhimu sana. Lakini Yohana hakutenda muujiza wowote—tazama Yohana 10:41, kwa hivyo hudumu ya Yohana haikujenga sehemu yoyote ya thibitisho. Mungu alitenda kupitia kwa Kristo katika kazi hizo zenye nguvu, kwa nusu juma, na kupitia kwa mitume nusu hiyo nyingine, ambao walikuwa wamepewa kazi ya kipekee, na ambao walikuwa wamehitimu kikamilifu, na hiyo ilikuwa kushuhudia kuhusu kazi na Kufufuka kwa Bwana wetu--tazama Luka 1:2; Yohana 15:27; Luka 24:48; Matendo 1:8, 21,22; 2:32; 3:15; 10:36,42; 1 Yohana 1:1,3. Mashahidi hawa wote isipokuwa mmoja waliitwa kwa utaratibu na kuhitimu, kwa kuwa na Kristo tangu mwanzo wa huduma, baada ya Yohana kutiwa gerezani. Lakini Paulo alipobadilishwa, na akapokea mpango wake wa injili kwa watu wa mataifa, shahidi wa kipekee aliitwa kusimama.

Hawa wote walishuhudia ukweli mmoja tukufu na wa msingi, kwamba Yesu Kristo alikuwa amefufuka katika wafu. Gal. 1:10-12; 1 Kor. 15:1-9. Halikuwa na mitume suala la imani kwamba Kristo alikuwa amefufuka, mbali suala la ufahamu. Walikuwa wamemwona, kumguza, na kunena naye, walikuwa wamekula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake, na walikuwa wamepokea amri kutoka kwake kushuhudia kuhusu mambo haya. Kwa kufanya hivyo walithibitisha agano, au, kwa njia nyingine, kuanzisha injili, juu ya kufufuka kwa Kristo, ambako ni msingi wa imani na tumaini kwa wana wote wa Mungu. Lakini ushuhuda huu pekee haukutosha kukuza ukweli kwamba Yesu alikuwa amefufuka katika wafu. Kwa hivyo tunaambiwa, Marko

16:20, "Kisha wanafunzi Wake wakatoka, wakahubiri kila mahali, naye Bwana akatenda kazi pamoja nao na kulithibitisha neno Lake kwa ishara zilizofuatana nalo." Pia tazama Ebr. 2:3,4. Shahidi wa mwisho, ambaye ni Paulo, alikuwa ameitwa, na alikuwa ametoa ushuhuda wake, uliothibitishwa na miujiza, injili kama mfumo takatifu wa imani, tumaini, na upendo ulianzishwa kwa msingi wake wa kweli; kwa namna nyingine, agano lilithibitishwa. Paulo alibadilishwa katika majira ya vuli ya A.D. 34. Kama Yesu Kristo alivyo sulubiwa katikati ya juma, na katika siku ya pasaka, ambayo ilikuwa siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza, ilifuata kwamba juma lilianza katika mwezi wa saba wa A.D. 27, na likaisha katika mwezi wa saba wa A.D. 34. Huu ulikuwa utimilifu wa majuma sabini. Kuanzia hapo, miaka 1810 ilisalia kukamilisha siku 2300. Na kutoka kwa mwezi wa saba wa A.D. 34, miaka 1810 iliendelea hadi mwezi wa saba wa A.D. 1844.

## Mfano.

Sheria ya Musa ilikuwa na kivuli cha vitu vizuri vijavyo; mfumo wa takwimu au mfano ukionesha Kristo na ufalme wake. Tazama Ebr. 10:1; Kol. 2:16,17. Kila kitu ambacho kilikuwa kwenye sheria kilikuwa kitimizwe naye. Katika Matt, 5:17,18, Yesu anasema, "Msidhani kwamba nimekuja kuondoa Torati au Manabii, sikuja kuondoa bali kutimiza. Kwa maana, amin, nawaambia, mpaka mbingu na dunia zitakapopita, hakuna hata herufi moja ndogo wala nukta itakayopotea kwa namna yo yote kutoka kwenye Torati mpaka kila kitu kiwe kimetimia." Bwana wetu katika kuja kwake mara ya kwanza, alipokufa msalabani, alianza kutimiza mifano iliyokuweko kwenye sheria; kama Kuhani wetu Mkuu bado anaitimiza; na atakapokuja mara ya pili, atakamilisha kuitimiza. Hakuna hata nukta moja itakosa kutimia, katika kiini kilichotabiriwa, au katika wakati uliowekwa dhahiri kutazama maadhimisho ya mifano. Kwa kuwa Mungu ni mweka wakati sahihi. Tazama Matendo 17:26,31; Ayubu 24:1; Lawi. 23:4,37. Mafungu haya yanaonyesha kwamba wakati ni hoja muhimu katika sheria ya Bwana; kwa hivyo mifano na mifano-akisi lazima iwe na mlingano sawa kulingana na wakati. Mfano mmoja ambao ulitimizwa katika Kristo ulikuwa kuuawa kwa Mwana-kondoo wa Pasaka. Huyu alichinjwa katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza, Tazama Lawi. 23:5. Kutoka Kut. 12:6 tunajifunza kwamba mwana-kondoo aliuawa jioni. Maelezo

kiasi yanatupa utoaji halisi kutoka kwa Waebrania, "katikati ya jioni mbili." Joseph Frey, Myahudi aliyeongolewa, katika kazi yake juu ya Pasaka, anasema alasari au jioni ya siku ilikuwa imegawanywa katika sehemu mbili na wao, jioni ndogo au ya awali na jioni kuu au ya mwisho. Sehemu ya kugawanya hizo mbili ilikuwa saa tisa alasiri, saa ya tisa ya siku. Yesu alikufa msalabani, siku hiyo hiyo na saa hiyo hiyo. Tazama Marko 15:33-37. Kwa hivyo Kristo pasaka yetu alisulubishwa kwa ajili yetu. Hakuna hata nukta moja ya sheria ilikosa kutimia hapa. Wakati ulikuwa ukionekana madhubuti. Katika Lawi. 23:6,7 tunafahamishwa kwamba siku baada ya Pasaka ilikuwa Sabbato ya kipekee; na katika fungu la 10 na 11, ni amri kutoa malimbuko ya mavuno ya mganda baada ya Sabbato. Hili lilikuwa mfano wa kufufuka kwa Kristo. na katika siku hiyo hiyo, yaani, siku baada ya Sabbato aliivunja minyororo ya kaburi, na akafufuka mshindi, sampuli ya mazao ya siku za usoni, limbuko la waliolala. Tazama 1 Kor. 15:20-23. Tena, katika Lawi. 23:15,16, tuko na wakati wa sikukuu ya majuma, au, kama inavyoitwa, Pentekosti, ambayo ni siku ya hamsini. **Hii ilikuwa ukumbusho wa kushuka kwa Mungu juu ya mlima Sinai wakati wa kutoa sheria; na ilitimizwa, kama tunavyojifunza kutoka kwa Matendo 2:1-4**, Roho Mtakatifu aliposhuka kama upepo wenye nguvu na kasi, na kama ndimi za moto, ambaye kwake mitume walijazwa na nguvu kutoka juu, akiwafanya kuhitimu kwenda nje na kutangaza kazi kuu ambayo Bwana alikuwa amewapa, kuhubiri injili kwa kila kiumbe.

Kwa hivyo tunaona kwamba mifano hiyo ambayo inaashiria matukio yanayohusiana na kuja kwa kwanza kwa Bwana wetu yalitimizwa halisi katika wakati wa kuadhimishwa kwake. Na yule ambaye sio kipofu kwa hiari lazima aone, na kuhisi pia, kwamba yale ambayo bado hayajatimizwa yatatimizwa pamoja na maadhimisho madhubuti kuhusiana na wakati. Sio hivyo tu, bali Kristo anadhibitisha tetesi hii kutoka kwa ulinganishi kwa kusema kwamba Jodi moja au nukta haitaondolewa katika torati, hadi yote yatimizwe. Mifano hiyo ambayo ilikuwa iadhimishwe katika mwezi wa saba, bado kamwe haijahitimishwa katika mfano-akisi.

Siku ya kwanza ya mwezi huo, kama tunavyojifundisha kutoka kwa Law. 23:23-25, ilikuwa ukumbusho wa kupuliza tarumbeta. Tazama Zab. 81:3: "Pigeni panda mwandamo wa mwezi, Wakati wa mbalamwezi, sikukuu yetu." Tazama pia Ufu. 10:7-11: "Lakini katika siku zile ambazo huyo malaika wa

saba atakapokaribia kuipiga hiyo tarumbeta yake, siri ya Mungu itatimizwa, kama vile alivyowatangazia watumishi wake manabii." Siku ya kwanza ya mwezi wa saba, miaka 6000 ikiwa imekamilika, Sabbato kuu ya milinia itaanzishwa, kwa sauti ya tarumbeta ya saba. Aina nyingine inatolewa katika Lawi. 23:26-32, hiyo ni, siku ya upatanisho, siku ya kumi ya mwezi wa 7, ambayo kuhani mkuu aliendà patakatifu mno pa hema, akiwasilisha damu ya waathiriwa mbele ya kiti cha rehema, ambapo baadaye siku hiyo hiyo alitoka na kubariki mkutano wa Waisraeli uliokuwa ukimngojea. Tazama Lawi. 9:7, 22,23,24, na Lawi. Sura ya 16.; Ebr. 5:1-6, na 9:1-12,27,28. Sasa hoja muhimu katika mfano huu ni ukamilifu wa upatanisho wakati wa kuja kwa kuhani mkuu kutoka kwa patakatifu. Kuhani mkuu alikuwa mfano wa Yesu kuhani wetu mkuu; patakatifu mno mfano wa mbinguni yenyewe; na kutoka kwa kuhani mkuu ni mfano wa kuja kwa Yesu mara ya pili kuwabariki watu wake wanao msubiri. Kama hili lilivyokuwa katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, hivyo katika siku hiyo kwa hakika Yesu atakuja, kwa sababu hakuna hata nukta moja ya sheria itakosa kutimia. **Sikukuu ya vibanda, ambayo ilianza siku ya kumi na tano ya mwezi wa saba, (tazama Lawi. 23:33-43,) ilikuwa mfano wa karamu ya harusi ya Mwana-kondoo; ambayo itasherehekewa katika Yerusalemu mpya,** hema ya Mungu ambayo itakuwa pamoja na wanadamu. Katika Lawi. 25:8-13,23,24, **tunapata kwamba katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, katika mwaka wa kumi na tano, tarumbeta ya yubilee daima ilipulizwa na wokovu ulitolewa kwa nchi yote.** Mtu yeyote asome kwa makini uhusiano wa suala hili, na hakika lazima aone kwamba huu ni mfano unaogusa zaidi wa ukombozi wa utukufu wa watu wa Mungu, na wa uumbaji wote ambao sasa unaugua chini ya laana, wakati ambao Mkombozi atakuja zayuni, na kukamilisha wokovu wa miili ya watakatifu wake wote, na ukombozi wa miliki iliyonunuliwa. Tazama Rum. 8:19-23; Efe. 1:9-14. **Bwana wetu kwa hivyo atakuja, kwa mshangao kwa wale wote wakaao juu ya dunia, na kwa ukombozi wa wale wamtafutao kwa kweli, katika siku ya kumi ya mwezi wa saba ya mwaka wa yubile**: na huo ni mwaka uliopo, 1844.

"Wasipowasikia MUSA na MANABII, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu."

# Kelele Ya Usiku Wa Manane Ya Kweli

"Katika harakati zote kuu za kidini tangu siku za mitume, hakuna ambayo imekuwa huru kutoka kwa kasoro za wanadamu na hila za Shetani kuliko ilivyokuwa ile ya vuli ya 1844. Hata sasa, baada ya miaka mingi kupita, wote ambao walishiriki katika harakati hiyo na ambao wamesimama dhabiti juu ya jukwaa la kweli bado wanahisi athari takatifu ya kazi hiyo ambayo imebarikiwa na kushuhudia kwamba ilikuwa ya Mungu." Great Controversy, ukurasa 402.

"Nilipokuwa nikiomba katika madhabahu ya familia, Roho Mtakatifu alikuja juu yangu, na nilionekana kuinuka juu zaidi, juu kuliko ulimwengu wa giza. Niligeuka kutafuta Waadventista ulimwenguni, lakini sikuwaona, ndipo sauti ikasema kwangu, "Angalia tena, na angalia juu kidogo." Katika hili niliyainua macho yangu, na nikaona njia iliyonyooka na nyembamba, ikiwekwa juu ya ulimwengu. Juu ya njia hii Waadventista walikuwa wakisafiri kwelekea kwenye mji, ambao ulikuwa mbali kwenye mwisho wa njia. **Walikuwa na mwanga uliong'aa uliowekwa nyuma yao kwenye mwanzo wa njia, <u>ambao malaika aliniambia ulikuwa kelele ya usiku wa manane</u>. Nuru hii iliangaza njia yote na kutoa nuru kwa miguu yao ili kwamba wasijikwae**. Kama wangeweka macho yao kwa Yesu, ambaye alikuwa mbele yao, akiwaongoza kuelekea kwa mji, wangekuwa salama." Early Writings, Ukurasa 14.